**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**<u>HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA</u>**

**SHULE YA SEKONDARI RUDEWA,**
**S.L.P 261,**
**KILOSA.**
**<u>10-12-2019</u>**

**KUMB / RUD SS /ADM /VOLI /......................**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

....[illegible]..........BAYORI..........K[illegible].......

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUDEWA KWA MWAKA WA MASOMO 2020.</u>**

Husika na mada tajwa hapo juu.

Ninayofuraha kukutaarifu kuwa mwanao mtajwa hapo juu Amechaguliwa Kujiunga Na Kidato Cha Kwanza katika Shule Ya Sekondari Rudewa. Kuchaguliwa kwake kumetokana na juhudi na uwezo alio onyesha katika masomo yake. Hivyo naamini kuwa ataendelea pia na juhudi hizo za kimasomo katika Elimu ya Sekondari.

Shule itafunguliwa kwa muhula wa kwanza tarehe **06-01-2020**, Mwanao anatakiwa kuripoti siku ya kufungua shule , Afike Saa **1:00** Asubuhi bila kuchelewa.

1. **<u>MAVAZI NA SARE ZA SHULE</u>**
   I. Sare za shule hii Ni Suruali Rangi ya Kijani kwa Wavulana/ Sketi Rangi ya Kijani kwa wasichana na wote Shati Nyeupe ya mikono mifupi. Ili Mwanafunzi awe msafi anatakiwa awe na suruali / Sketi mbili na shati pea mbili kwa kila mmoja.
   II. Mshono wa suruali usiwe ule wa kubana ( modo) na wenye turn up chini na Wasichana sketi zisizo shika mwili (kubana) na ndefu zenye kufunika miguu.
   **NB: SURUALI AMBAZO ZIMEBANA(MODO) NA HAZINA TURN UP NA SKETI FUPI KWA MWANAFUNZI HAZITAKIWI, KWA ATAKAYE KIUKA AGIZO HILI TUTACHANA SURUALI/ SKETI ILI AKAREKEBISHE KWA GHARAMA ZAKE.**
   III. Wanafunzi wanaovaa hijabu ifanane na shati la shule (Nyeupe) isiyo na urembo wowote kichwani wala chini.
   IV. Sare ya viatu viwe vya ngozi na vyenye kamba , siyo vile vya kutumbukiza kwa Wavulana na Wasichana , Pia viatu kwa wasichana visiwe vya Kisigino kirefu.
   V. Soksi Pea mbili Nyeusi kwa Wavulana na Nyeupe kwa Wasichana, kila mwanafunzi awe nazo ili kuwezesha usafi binafsi.
   VI. T-shirt zinapatikana shuleni, Nembo za mashati hutolewa pia shuleni.
   VII. Tai iwe rangi ya kijani kama ilivyo sketi na Suruali , tai zinapatikana kwa fundi atakayeshona sketi / suruali.
2. **<u>VIFAA VINGINE</u>**
   I. Vifaa vya darasani, aje na mkebe (mathematical set) moja, madaftari makubwa 18 kwa matumizi ya darasani na mazoezi na mitihani Mbalimbali , Pamoja na Kalamu za wino na Penseli.
   II. Aje /Awe na begi la kubebea madaftari yake, mifuko ya Rambo / karatasi na aina nyingine ya vibebeo havikubaliki shuleni , isipokuwa begi la kubeba mgongoni tu.
   III. Siku ya kuripoti shule aje na **fyekeo , ndoo moja ndogo na fagio la Chelewa** kwa ajili ya usafi wa mazingira awapo shuleni. Vifaa hivi vyote vikabidhiwe shule siku ya kuripoti.
3. **SHERIA NA KANUNI MBALIMBALI ZA SHULE ATAZIKUTA SHULENI KATIKA MBAO ZA MATANGAZO NA MADARASANI.**
4. **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE PIA ATAYAKUTA SHULENI KATIKA MBAO ZA MATANGAZO NA MADARASANI.**

**NB: Siku ya kuripoti Mwanafunzi aje na Mzazi / Mlezi wake pamoja na fomu hii na Medical Examination Sheet /Certificate.**

Scanned with CamScanner

## APENDIX "A"

FROM RUDEWA SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 261,

KILOSA.

DATE: ....................................

REF:

TO MEDICAL OFFICER

.......................................................................

MR/MRS/MISS.......................................................................

Please examine the above name as to his/her physical and fitness for full time studies. The examination should include the following category or subcategory of which will also render a student ineligible for studies.

1. (i)Eye Sight..........................................

   (ii)Hearing..........................................

   (iii)Speech..........................................

   (iv)Limbs..........................................

   (v)Venereal Disease..........................................

   (vi)Leprosy ..........................................

   (vii)Epilepsy..........................................

2. Other Serious Disease..........................................................
3. Pregnancy for girls student..........................................................

**Date:**......................................

**Signature :**..................................

## APENDIX "B"

**MEDICAL CERTIFICATE**

***(To be completed by a Government Medical officer.)***

I have examined the above named student and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit to be a full time student.

Other explanation ..........................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

**Medical doctor:**..........................................................

**Signature:**..........................................................

**Date:**..........................................................

Scanned with CamScanner